



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA MADINI  
TUME YA MADINI



Unapojibu tafadhali taja:  
Kumb. Na. HA.123/457/20443/09

16 Oktoba, 2024

Mkuu wa Wilaya,  
Wilaya ya Dodoma Mjini,  
S. L. P. 1246,  
DODOMA.

Yah: UTAMBULISHO

Kichwa cha habari cha husika.

Napenda kumtambulisha kwako M/S **William Vedastus Mathayo** kuwa ni mmiliki wa leseni ndogo za uchimbaji madini Namba **PML4507DOM** na **PML4508DOM** zilizotolewa tarehe 28/08/2024 kwa Mujibu wa Sheria ya Madini Sura 123. Kwa mujibu wa maombi yaliyowasilishwa na mmiliki wa leseni, leseni hizi ziko eneo la **Kikombo** Wilaya ya Dodoma Mjini Mkoa wa Dodoma.

2. Aidha, mmiliki wa leseni ndogo anawajibika kufanya yafuatayo kwa Mujibu wa Sheria ya Madini tajwa hapo juu;

- I. Kabla ya kuanza shughuli za uchimbaji madini, mmiliki wa leseni anapaswa kupata ridhaa ya mmiliki halali wa ardhi ya eneo husika kwa mujibu wa Kifungu cha 95 cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Marekebisho yake;
- II. Kutambua na kuweka mipaka ya kuonekana kwenye eneo la leseni zake kabla ya kuanza shughuli za uzalishaji;
- III. Kujitambulisha kwa Ofisi za Mkuu wa Wilaya Dodoma Mjini na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma Mjini. Ofisi ya Mkurugenzi itampatia utambulisho kwenye Serikali ya Ngazi ya Kata na kijiji husika kwa mujibu wa Sheria na taratibu husika;
- IV. Kuchangia kwenye Halmashauri 0.3% ya uzalishaji kama *service levy*, na kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo ya jamii katika eneo/kijiji/Mtaa anapofanyia uchimbaji kadri awezavyo na kutegemea kipaumbele cha mahitaji ya eneo husika (*Corporate Social Responsibility*) kwa mujibu wa Kifungu cha 105 cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Marekebisho yake;
- V. Mmiliki wa leseni atapaswa pia kuandaa taarifa ya Mpango wa utunzaji mazingira (*Environment Protection Plan-EPP*) ndani ya miezi mitatu baada ya kupata leseni na

kabla ya kuanza kazi ya uchimbaji wa madini katika eneo lake kwa mujibu wa Kanuni Na 3 na 4 za Kanuni za Madini (Uhifadhi Mazingira kwa Uchimbaji Mdogo) za mwaka 2010; na

VI. Kuzingatia Sheria, Kanuni na miongozo husika na eneo zitakapofanyika shughuli za uchimbaji mdini.

3. Nawasilisha.



Msafiri A. Kussa

Kny: **KATIBU MTENDAJI**  
**TUME YA MADINI**

**Nakala:** Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Jiji Dodoma (M) *(Kwa utambulisho ngazi ya Kata na Kijiji)*

**William Vedastus Marthayo (Mob#+255 782 696 188)**

---

Afisa Madini Mkazi, S.L.P. 903, Dodoma, Simu: +255 0262322407, Nukushi: +255 026 2322407, Barua pepe: [dodoma@tumemadini.go.tz](mailto:dodoma@tumemadini.go.tz), Tovuti: [www.tumemadini.go.tz](http://www.tumemadini.go.tz)